



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA

MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA UONGOZI WA HALMASHAURI (CMT)
KILICHOFANYIKA TAREHE 25/10/2021 KATIKA UKUMBI WA
MIKUTANO WA HALMASHAURI.

Wajumbe waliohudhuria

- | | | |
|--------------------------------|---------------------------------------------------|----------|
| 1. Frank F. Chonya | -Mkurugenzi Mtendaji | - M/Kiti |
| 2. Ndg. Mohamed R. Muhidini | -Mkuu wa Idara Utumishi na Utawala | - Katibu |
| 3. Ndg. Joseph Mdasia | -K/Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara | |
| 4. Ndg. Solomoni Masangya | -Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili | |
| 5. Ndg. Rashid Namkulala | -Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii | |
| 6. Ndg. Jitetee Mbonde | -K/Mkuu wa Kitengo cha Tehama | |
| 7. Adv. Albert Mombeki | -K/Mkuu wa Kitengo cha Sheria | |
| 8. Dkt. Salvio Wikesi | -Mkuu wa Idara ya Afya | |
| 9. Ndg. George R. Mbesigwe | -Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi | |
| 10. Eng. Frank M. Kiunga | -K/Mkuu wa Idara ya Ujenzi | |
| 11. Ndg. Tuntufye C. Mwamwaja | K/Mkuu wa Idara ya Eimu Sekondari | |
| 12. Ndg. Nolasco D. Kilumile | -K/Mkuu Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | |
| 13. Ndg. Msafiri Ngai | -Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi | |
| 14. Ndg. Salim S. Msangi | -K/Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi | |
| 15. Ndg. Didas John. M | -Mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa ndani | |
| 16. Ndg. Fundikira L. Masamalo | -Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji | |

Sekretarieti

- | | |
|----------------------------|------------------------|
| 1. Ndg. Selemani Ng'ambage | -Mwandishi wa Mikutano |
|----------------------------|------------------------|

AGENDA NA. CMT.2021/10/1 KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 3.40 Asubuhi.

AGENDA NA. CMT.2021/10/2 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA SHILINGI 1,490,000,000.00 ZA UVIKO-19 KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UJENZI KATIKA SEKTA ZA ELIMU MSINGI, SEKONDARI NA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

Mkuu wa idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji alitoa taarifa kuwa halmashauri ya wilaya ya Ruangwa imepokea jumla ya shilingi 1,490,000,000.00 za uviko-19 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kwa sekta za elimu msingim sekondari na afya, ambapo shilingi 360,000,000.00 ni kwaajili ya ujenzi wa madarasa 18 kwa shule shikizi 7, shilingi

660,000,000.00 ni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 33 kwa shule za sekondari 14, shilingi 300,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la huduma ya dharula katika hospili ya wilaya na shilingi 90,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 1 ya watumishi (3 kawa 1) katika zahanati ya chikundi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Wajumbe wamepokea taarifa na kuipongeza serikali kwa jitihada zake kubwa za kutatua changamoto nyingi zinazokumba jamii pamoja na kuwezesha maendeleo, wajumbe waliweka mikakati madhubuti itakayotumika katika utekelezaji wa miradi ya Uviko-19 kwa kupendekeza yafuatayo:-

1. Kuhakikisha vifungu vya fedha zote vinasoma kwa wakati na kuanza utekelezaji haraka iwezekanavyo.
2. Kuunda kamati mbalimbali zitakazosimamia utekelezaji wa miradi kwa kanda.
3. Kuwaongezea nguvu walezi wa kata zilizopokea fedha za utekelezaji wa miradi ya Uviko-19 kwa kuhamishia/ kuongeza walezi wa kata kutoka katika kata nyingine.
4. Kuwapanga watumishi kwa kata ili kuwezesha usimamizi wa kina na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi.

Wajumbe wote walikubaliana kwa pamoja na kuahidi kutoa ushirikiano wakati wote kwa asilimia mia moja.

AGENDA NA.CMT.2021/10/3 KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 06.30 mchana.

UMETHIBITISHWA



MWENYEKITI



KATIBU

26/10/2021

TAREHE